

**KAULI YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO, DKT.
H.G. MWAKYEMBE (Mb) KUHUSU FURSA KWA WASICHANA KUJIPIMA
UWEZO KATIKA RIADHA ILI WAWEZE KUIWAKILISHA NCHI KATIKA
MASHINDANO YAJAYO YA KIMATAIFA YA JUMUIYA YA MADOLA,
OLIMPIKI, ALL-AFRICA GAMES NA MENGINEYO**

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) imeandaa mashindano ya riadha kwa Wasichana yatakayofanyika tarehe 25-26 Novemba 2017, Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mhe. Spika, lengo kuu la mashindano haya ni kutoa fursa kwa vijana wote wa kike nchini wenye vipaji katika riadha waweze kuonesha uwezo wao kwa kushindanishwa na wenzao ki-Wilaya na ki-Mkoa na hatimaye ki-Taifa jijini Dar es Salaam tarehe 25&26 Novemba, 2017. Watakaofikia au kukaribia viwango kimataifa, tutawalea ki-ufundi ili watuwakilishe katika mashindano yajayo ya kimataifa yakiwemo ya Jumuiya ya Madola (Australia 2018): All Africa Games (2019) na Olimpiki (Tokyo, Japan 2020) na mengine ya kimataifa. Mashindano haya ambayo yanafadhiliwa kitaifa na JICA yamepewa jina la “Women pre-Olympics Trials towards the 2020 Tokyo Olympics”, yatahusisha wilaya zote za Tanzania ambazo zitatoa wanariadha bora watano (5) na kiongozi au mwalimu mmoja wa michezo kwa kila Mkoa.

Mhe. Spika, utaratibu huu tunaoutumia mwaka huu utasaidia sana nchi kuwa na uchaguzi mpana wa vipaji tulivyonavyo nchi nzima badala ya kutegemea uteuzi wa wanariadha wetu ufanywe na asasi chache za michezo jijini Dar es Salaam. Hivyo tutakuwa na jumla ya wanamichezo 186 katika mashindano hayo ambao watakapokuwa jijini Dar es salaam mpaka wanaondoka watahudumiwa na JICA kwa kushirikiana na Wizara na taasisi zake.

Mhe. Spika, historia inaonyesha miaka ya 60, 70 na 80 tulikuwa na wanariadha wazuri sana wa kike kama akina Mwinga Mwanjala, Nzaeli Kyomo, Restituta Joseph, Rwiza John n.k. ambao walililetea taifa letu sifa na heshima kubwa katika michezo. Vilevile historia inaonesha kuwa medali ya kwanza kimataifa ya riadha ililetwa nchini na mwanamama Bi. Theresia Dismas ambaye alishinda michezo wa kurusha kisahani mwaka 1965, (miaka 4 tu baada ya Uhuru) kwenye mashindano ya All-Africa

Games nchini Congo Brazaville. Rekodi hii iliyotukuka ya michezo, haikuendelezwa baadaye kutokana na kukosekana kwa msukumo stahili wa michezo ambao sasa tumeurejesha.

Mhe. Spika, ili kampeni hii ya kupata wanariadha bora wa kike nchini ifanikiwe, niruhusu kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote wahakikishe kwamba wilaya zao zinafanya uteuzi wa wasichana bora kwenye riadha ndani ya wiki hii na ijayo ili kuipa mikoa muda wa kutosha mwishoni kufanya uteuzi wa wanariadha 5 na kiongozi (mwalimu) mmoja ambao watakaosafirishwa hadi Dar es Salaam kabla ya tarehe 25 Novemba, 2017, tayari kwa michuano hiyo. Ni matumaini ya Wizara kwamba Waheshimiwa Wabunge watahimiza na kuhakikisha kuwa Wilaya zinatekeleza wajibu wao katika hili na vyama vyta riadha vyta mikoa na kamati za michezo za mikoa vinashirikiana kwa karibu kufanya uteuzi wa wanariadha bora bila upendeleo au uonevu na kuwasafirisha hadi Dar es Salaam ambako maandalizi ya kuwapokea na kuwahifadhi yanafanyika.

Mhe. Spika baada ya kuyasema hayo, ninaomba kuwasilisha.

Dkt. Harrison George Mwakyembe (Mb),
WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

14 Novemba, 2017